OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI LUMULI

**MKOA WA IRINGA**

**SANDUKU LA POSTA 2436**
**IRINGA**
**TANZANIA**

SIMU + ***225 763 264 594/0621 372 737***
Email: slumuli@yahoo.com

**MAJINA KAMILI ……..……..**

**SHULE YA MSINGI ALIYOHITIMU ……..**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI.**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Lumuli mwaka 2021. Unatakiwa kufika shuleni tarehe …… bila kukosa kwa ajili ya usajili tayari kwa masomo. Kwa barua hii naambatanisha fomu za maagizo maalum unazotakiwa kuzijaza utakapokuwa unamleta mwanao.

1. Fomu ya kukubali nafasi ya kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondali Lumuli
2. Fomu ya kupima afya yako ( mtoto apimwe na fomu iwe na saini ya mganga mkuu wa mkoa au wilaya sio zahanati/kituo cha afya)
3. Uje na cheti cha kuzaliwa /ikishindikana uje na cheti cha kuapa mahakamani (Affidavit)

Fomu hizo unatakiwa kuja nazo siku ya kuripoti zikiwa zimejazwa vipengele vyote ili kuepusha usumbufu. Mkuu wa shule/ walimu na wafanyakazi wote wa Shule ya Sekondari Lumuli wanatarajia uwe mwanafunzi mtii/ nadhifu /mwaminifu/ aliye tayari kusoma kwa bidii yake yote / na kushiriki kazi zote za darasani na nje kama utakavyopangiwa na uongozi wa shule.

❖ ***Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki AU kuja na simu shuleni.***

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI LUMULI**

……..…

HERY J. LUKUVI

Mkuu wa Shule

## MAZINGIRA YA SHULE

Shule ipo katika kijiji cha Muwimbi, kata ya Lumuli, tarafa ya Kiponzero wilaya ya Iringa mkoani Iringa **kilometa 3 kando ya barabara kuu Mbeya - Dar –es – Salaam. Kwa wanaotoka mbali shukia stendi ya ulete,** Lumuli ni shule ya kutwa na ni mchanganyiko (Wavulana na wasichana) kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha Nne. Aidha kwa wazazi wote wa Wanafunzi wanaotoka nje ya kijiji cha muwimbi unashauriwa kuhusika kikamilifu kumtafutia mtoto wako mahala salama pa kuishina usiache mtoto ajitafutie kwani kumbuka utakuwa mbali naye. Mwenyeji wako ambaye mtoto wako ni mpangaji wake , hakikisha ni mtu atakaye simamia malezi na nidhamu ya mwanao akiwa nyumbani baada ya masomo badala yako kulea mwanao ukiwa mbali. Pia unashauriwa kujenga tabia ya kumtembelea mwanao ili kujua maendeleo yake kitaaluma na kitabia awapo shuleni na nyumbani.

## MAHITAJI YA SHULE

a) **WASICHANA**
1. Sketi mbili ndefu zinazovuka magoti, ikiwa rangi ya kijani jeshi 1 na rangi ya khaki 1
2. Mashati mawili meupe, ikiwa mikono mirefu 1, na mikono mifupi1 ***(Angalia Tanibihi namba (i) hapo chini )***
3. Soksi nyeupe ndefu (stocking ndefu) jozi mbili.
4. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi (jozi mbili) vinavyofungwa kwa kamba.
5. Raba jozi moja aina yoyote kwa ajili michezo.
6. Track suti rangi ya **bluu bahari** kwa ajili ya michezo (isiwe ya kubana)
7. Sweta rangi ya bluu yenye mpasuo wa **v** juu ya kifua

**b) WAVULANA**
1. Suruali mbili, rangi ya khaki 1 na kijani 1 upana wa suruali chini iwe **nchi 18** na tan up (zitapimwa)
2. Mashati mawili meupe, ikiwa mikono mirefu 1 na mikono mifupi 1 ***(Angalia Tanibihi namba (i) hapo chini )***
3. Soksi jozi mbili nzito na ndefu rangi nyeusi.
4. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi (jozi mbili) vinavyofungwa kwa kamba.
5. Raba jozi moja aina yoyote kwa ajili ya michezo.
6. Track suti rangi ya **bluu bahari** kwa ajili ya michezo (isiwe ya kubana)
7. Sweta rangi ya bluu yenye mpasuo wa **v** juu ya kifua.

TANIBIHI: ***i)*** Lebo rangi ya kijani jeshi ibandikwe kwenye shati la mikono mirefu na khaki iwekwe kwenye shati la mikono mifupi

***ii)*** Vitu vyote vilivyoagizwa hapo juu vitakaguliwa siku ya usajili wa Mwanafunzi hivyo unashauriwa kuzingatia maagizo kupunguza usumbufu usio wa lazima.

**MAHITAJI MENGINE**

Daftari 10 (***counter book Quire three/ four***) Daftari ndogo za msomi 10, mathematical set 1, kamusi (Dictionary) ya Kiswahili-Kiingereza, (Vyote hivi ni kwa ajili yake mwenyewe)

Baadhi ya sheria na kanuni muhimu za shule unazotakiwa kuzielewa na kuzifuata.

**A. MWANAFUNZI**

1. Unatakiwa kusimama na kusalimia mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Hutakiwi kutumia lugha mbaya, chafu wakati wowote unapowasiliana.
3. Unatakiwa kuonesha heshima kwa wafanyakazi wote wa shule kama walezi wako.
4. Unatakiwa kuonyesha ushirikiano kusaidia katika kazi.
5. Utathamini na kuheshimu kazi za aina zote hapa shuleni.
6. Huruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-
   - ❖ Kuvuta sigara
   - ❖ Kufuga kucha ndefu, kupaka rangi, kuwa na nywele ndefu zisizo katika hali ya usafi
   - ❖ Kufuga ndevu
   - ❖ Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
   - ❖ Kuvaa milegezo (kata K au mavazi yanayoangaza, kubana, sketi fupi kwa wasichana n.k)
   - ❖ Kupiga au kupigana (kugombana)
   - ❖ Kuandika maandishi yoyote katika majengo, maeneo ya shule na popote bila kibali toka uongozi wa shule.
7. Unatakiwa kufika mara moja na kukimbilia aliko mkuu anayekuita.
8. Unatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa,na fedha ya Taifa.
9. Untakiwa kuwahi shuleni kulingana na ratiba ya shule.
10. Unatakiwa kulinda mali ya shule, aidha mzazi/mlezi atawajibika utakapotokea uharibifu/upotevu wa mali ya shule atakaoufanywa na mwanafunzi.
11. Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa bila kukosa.

**B. Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa shule**

1. Wizi
2. Uasherati,ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi mabaya ya dawa za kulevya.
4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai. (Kuua au kushiriki kosa la unyang'anyi)
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule/umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, na fedha ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma au kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi. (Kugoma)
14. Utoro

**NB**:*Unatakiwa kuyasoma kwa makini maelekezo hayo na kuyaelewa na hivyo kuwa mwanafunzi aliye msitari wa mbele kutekeleza taratibu za shule kwa manufaa yako, shule,jamii na Taifa kwa ujumla.*

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi……..msichana/mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha…….. mwaka…….katika shule ya Sekondari Lumuli na nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi kwa ujumla. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo yangu pamoja na kazi za kujitegemea.

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi……sikubali/ninakubali mtoto wangu kujiunga na Shule ya Sekondari Lumuli kidato cha kwanza mwaka 2020 na ninaahidi kutompatia/kumpatia mahitaji yote muhimu kama ilivyo katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule (Joining instruction) ninakuhakikishia kuwa sitashirikiana/nitashirikiana na uongozi wa shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni:
…….
.....
.....
.....
.....

SIMU ……

Sahihi…….. Tarehe…….....……

*JAZA FOMU HII NA KUIRUDISHA SHULENI*

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI LUMULI

SLP 2436,

IRINGA

TAREHE …….

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……..……tarehe ya kuzaliwa ……
2. Kabila ……. Taifa ……
3. Dini na dhehebu …….……...……
4. Jina la Baba …….…… Simu ……
5. Anwani ya Baba / Mlezi ……...……
6. Kazi ya Baba/Mlezi …….……..
7. Jina la Mama …….……..…….Simu …….…….....
8. Kazi ya Mama …….……..
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana ……...……
10. Jina na anwani ya mzazi/mlezi wako……...……..
11. Ndugu wa karibu ..……..anwani…… simu …….
12. Ndugu wa karibu ..…..……..anwani……...…… simu …….
13. Ndugu wa karibu …….anwani.……...…… simu …….
14. Ndugu wa karibu …….anwani.……...…… simu …….

**NB**: Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapo juu ni za kweli na ni sahihi kabisa.

Saini ya Mwanafunzi ……...…… Tarehe ……...……..

Saini ya Mzazi/mlezi …….…… Tarehe ……

MINISTRY OF EDUCATIONAL AND VOCATIONAL TRAINING

LUMULI SEC. SCHOOL

P.O .BOX 2436,

IRINGA

DATE ……..

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

[To be completed by a Medical Officer in respected of all form I entrants]

Pupils full name ……

Age ……

Blood examination ……

Stool examination …….

Syphilis and other Venerial diseases test ……

T.B test …….

Eye test ……..

Ears test …….

Spleen ……....

Abdomen ……...

Urine for planio test …….

Test for pregnancy ……

ADDITIONAL INFORMATION

[If any] eg Physical defects, impartments eg arn legrets infections chronic or family diseases etc ……
…….....

I certify that the above is fit to pursue further studies in secondary education.

Station ……. Signature ……

Date ……. Designation ……